

Relaxer na Afya ya Msichana/Mwanamke

Clifford Majani

MANSHEP

<http://envaya.org/MANSHEP/news>

Relaxer ni dawa ya nywele inayofanya nywele za mtu mwenye ngozi nyeusi wa asili ya Afrika zilainike na kunyooka kama nywele za wazungu. Watu wengi hasa wanawake wanapenda kutumia *relaxer* ili nywele zao ziwe na mwonekano tofauti. Kihistoria matumizi ya *relaxer* yalianza kama matokeo ya watu weusi kubaguliwa. Watu weusi walipoona hivyo waliamua kuiga maisha ya kizungu ili kufanana fanana na wazungu kwa rangi ya ngozi na nywele ili wathaminiwe na kupewa upendeleo wa kupata fursa za mafanikio na watawala wetu enzi za ukoloni. Wakoloni waliwapendelea watu walioipokea kasumba hii kwa mikono miwili.

Siyo lengo langu kuingia kwa undani katika historia, ila ninajaribu kukupa picha ya chimbuko la matumizi ya kitumwa ya dawa zinazodhuru afya ya watu weusi kwa kiwango kikubwa. Pia kuititia mada hii najaribu kukupa uelewa ili unapofanya uchaguzi wa kutumia au kuacha, uchaguzi wako ujengwe katika uelewa sahihi na siyo katika mkumbo au msukumo wa kijamii unaowaona watu wasiotumia dawa hizi kama washamba.

Sayansi inaonyesha kuwa matumizi ya *relaxer* za nywele yanaweza kusababisha au kuongeza hatari ya kupata magonjwa ya moyo, kupungua kwa uwezo wa kiakili katika kufikiri na kupambanua mambo, kuungua kwa ngozi ya kichwa na muwasho wa ngozi. Matatizo mengine ni saratani ya matiti, mabonge katika mji wa mimba (*Leiomyomata*), upungufu wa kinga ya mwili na kubalehe mapema kwa wasichana. Katika utafiti uliofanywa na wanasayansi Lauren A. Wise na wenzake (Wise *et al.*, 2012) na kuchapishwa